

# **Tungo za Mrisho Mpoto: Sitiari ya Mwenendo wa Siasa na Utawala Nchini**

Manyuka Majuto Kapaya

## **Ikisiri**

Mrisho Mpoto ni mwanamuziki anayetumia mtindo wa kughani mashairi na kuimba nyimbo zenye mahadhi ya Kiafrika. Moja ya mambo yanayoupa upekee ushairi wake ni matumizi ya lugha fasaha na sanifu ya Kiswahili iliyojaa utajiri wa mbinu mbalimbali za kisanaa zikiwamo tamathali za semi, methali, nahau, misemo na mafumbo. Matumizi ya mbinu za kisanaa hasa tamathali za semi na ujenzi wa sitiari ya jumla katika tungo za Mpoto yamefanya mashairi yake kuwa magumu na yasioeleweka kirahisi. Kazi zake nyingi zinashughulikia siasa, jambo ambalo ni sehemu ya maisha ya kila mtu. Ni kusudi la makala haya kuchunguza namna ambavyo msanii amejenga sitari kudurusu mwenendo wa siasa na utawala nchini Tanzania. Kumekuwa na upungufu wa kazi zinazohakiki nyimbo za wasanii wa muziki kutokana na ukweli kuwa wahakiki wengi hupenda kuhakiki diwani, riwaya na tamthiliya ambazo zipo katika maandishi. Katika makala haya tutachambua nyimbo tatu za Mpoto: 'Njoo Uchukue', 'Sizonje', na 'Kitendawili'.

## **1.0 Utangulizi**

Katika makala haya tumejadili masuala yasiyopungua matano ambayo yanahusika na mada kwa namna moja ama nyingine. Kwanza kwa msaada wa kazi za wataalamu mbalimbali tumejadili dhana ya sitiari kama kipengele cha

tamathali za semi na pia tutaijadili sitiari katika dhana pana zaidi – yaani sitiari kama mtindo wa kiuandishi (utungaji). Mwishowe tumetoa maoni yetu juu ya dhana nzima ya sitiari. Tumefanya hivyo ili kujaribu kuipanua dhana ya sitiari katika hali ambayo itasaidia kuelewa mkondo wa uchambuzi wetu wa mada husika katika makala haya. Pili, tumefanya mapitio ya baadhi ya kazi za wataalamu walioshughulikia sitiari katika kazi za fasihi. Hili litafanyika ili kujenga mshikamano wa kitaaluma baina ya makala haya na kazi za wataalamu wengine. Tatu, tumeeleza historia fupi ya msanii yaani Mrisho Mpoto, ambaye kazi zake ndio kiini cha makala haya. Katika sehemu ya nne ya makala haya tumefanya uchambuzi wa kina wa sitiari ya mwenendo wa siasa na utawala nchini kama inavyojitokeza katika tungo za mashairi ya Mrisho Mpoto, na kwa kufanya hivyo tutakuwa tumetoa mchango wetu wa kitaaluma. Kazi za Mrisho Mpoto zitakazoshughulikiwa hasa ni tatu, yaani “Njoo Uchukue”, “Sinzonje” na “Kitendawili”. Sababu kuu ya kuteua kazi hizi ni ukweli kuwa ndizo kazi za msanii huyu za hivi karibuni na pia kwa mtazamo wetu kazi hizi zimejipambanua kuwa ni sitiari ya mwenendo wa siasa na utawala nchini. Sehemu ya tano itakuwa ni hitimisho ambapo tutatoa maelezo ya jumla juu ya kazi za Mrisho Mpoto.

## **2.0 Dhana ya Sitiari**

Mulokozi na Kahigi (1979) wanaeleza kuwa sitiari ni tamathali ambayo athari yake hutegemea uhamishaji wa maana na hisi kutoka katika kitu au dhana moja hadi kitu au dhana nyingine tofauti.

Samwel na wenzake (2013) wanaeleza kuwa sitiari huitwa pia istiara, istiari au jazanda. Hii ni tamathali ya semi (maneno, kirai au miundo) inayotumika kuumba picha fulani akilini inayotoa athari fulani kwa, au inayoamsha mwitikio fulani kutoka kwa hadhira. Wanatoa mifano ifatayo:

- i). Vero kwa urembo wake ni malaika
- ii). Gilo ana urefu wa mti wa mwanzi
- iii). Asha ana weusi wa mkaa

Mwakio (2016) anafafanua kuwa sitiari ni mlinganisho wa moja kwa moja ambao hutokea kwa kuhamisha maana ya sifa, tabia, sura, muundo au umbo fulani kutoka kwa kitu kimoja kwenda kwa kitu kingine.<sup>1</sup> Yeye amejaribu kuziainisha sitiari katika makundi kadhaa ikiwamo sitiari radidifu, sitiari sahili, sitiari hisimseto, sitiari za kikaida, sitari kuu na sitiari chakavu.

---

<sup>1</sup> Maelezo haya yamechukuliwa katika tasnifu ya uzamili ya Loyce Mwakesho Mwakio iliyowasilishwa katika Chuo Kikuu cha Nairobi, Oktoba 2016 kutosheleza mahitaji ya shahada ya umahiri.

Wataalamu hawa wote kwa ujumla wanaelekea kukubaliana mambo kadhaa; mosi, sitiari ni tamathali ya usemi, pili sitiari ni dhana ya ulinganishaji wa vitu au dhana mbili tofauti moja kwa moja, na tatu sitiari huibua picha fulani. Tunakubaliana kwa kiasi kikubwa na maelezo ya wataalamu hawa. Aidha, kwa ajili ya makala haya tutatoa maelezo juu ya dhana ya sitiari kadiri ya mtazamo wetu lakini kwa kuzingatia ufafanuzi wa wataalamu waliotutangulia.

Hivyo basi, tunaweza kusema kuwa sitiari ni moja ya tamathali za semi ambayo ni dhana inayodokeza ulinganisho fulani hivi kwamba jambo, kitu, dhana au mtu huzungumziwa ikimaanisha mtu, jambo, dhana au kitu kingine.

Sitiari ni ulinganisho wa vitu au dhana mbili ambapo huwa ni wa moja kwa moja toka kitu kimoja hadi kingine. Kwa kawaida sitiari huamsha mwitikio kwa hadhira kutokana na picha fulani inayokuwa imebebeba ndani yake. Aidha, sitiari huweza kuwa ni mtindo wa kiuandishi ambao hunuia kujenga uficho fulani wa maana inayokusudiwa katika kazi ya kifasihi. Sitiari huweza kujitokeza katika tanzu zote za fasihi. Kadhalika, inaweza kuwa katika namna tofautitofauti, mathalani, sitiari zilizozoeleka ambazo hutumia mbinu ya ulinganishaji wa vitu viwili pasi na kutumia maneno maalumu ya kulinganisha kama vile *kama, mithili ya, mfano wa* na kadhalika. Mifano ya sitiari za namna hii ni kama ifuatayo: *'Halima ni malaika' 'James ni simba', 'Mimi nina roho ya paka'*. Namna nyingine ya utokeaji wa sitiari ni ile itumiayo mbinu ya kutumia wahusika ambao huwa sitiari ya tabia au jambo fulani. Mfano mzuri wa sitiari za namna hii ni katika ngano nyingi za Kiafrika ambapo wanyama hutumika kama wahusika ambao huwa wamejengwa kisitiari wakiwakilisha tabia fulani za mtu au jamii fulani; sungura, kwa mfano, anatumika sana katika ngano za makabila mengi nchini Tanzania kuwakilisha watu wenye tabia ya ujanja,welevu na wakati mwingine ulaghai na utapeli. Fisi kwa upande wake hutumika kuwakilisha watu wenye tabia ya uroho, ulafi na wakati mwingine uvivu na ujinga. Vilevile, sitiari inaweza kujitokeza kwa njia ya matumizi ya mtindo wa uficho wa maana ya kazi nzima ya kifasihi, yaani tangu mwanzo wa hadithi au shairi hadi mwisho kazi hujengeka kisitiari hali ambayo hufanya kazi husika kuwa ngumu kueleweka kirahisi. Ili kuelewa kazi za aina hii huhitajika ujuzi wa kuzivunjavunja na kuzichambua sitiari husika. Mifano ni riwaya ya *Animal Farm* ya George Orwell (1945), tamthilya ya *Kongi's Harvest* ya Wole Soyinka (1965), riwaya fupi ya *Kusadikika* ya Shaaban Robert (1960), tamthiliya ya *Kaptula la Marx* ya Euphrase Kezilahabi (1978), ngano mbalimbali za Kiafrika kama vile *Ndege, Kazi kwa Mfalme, Sungura Aoa, Mama Mgumba* na kadhalika – hii ni mifano ya kazi za kifasihi zilizojengeka

kisitiari tangu mwanzo mwa hadithi hadi mwisho. Vilevile, zipo kazi za kishairi zinazofuata mkondo huu wa mtindo wa kisitiari, mfano mashairi mengi ya Kezilahabi katika diwani zake mbili za *Kichomi (1974)* na *Karibu Ndani (1988)* ni za kisitiari: “Kisu Mkononi”, “Nimechoka”, “Wimbo wa Mlevi”, “Ngoma ya Kimya”, “Hii Moja Hadithi”, “Mto wa Haki” na mengine mengi ni mifano ya kazi hizo.

### 3.0 Mapitio ya Kazi za Wataalamu mbalimbali

Wapo wataalamu mbalimbali ambao wamekwisha kushughulikia matumizi ya sitiari na tamathali nyingine za semi katika kazi za fasihi. Kombo (2014) amechunguza tamathali za semi ikiwamo sitiari katika mashairi ya magazetini. Anaeleza kuwa mashairi ya magazetini hutumia sitiari za aina mbalimbali kwa nia ya kuvyaza dhamira na kuziwasilisha kwa jamii iliyokusudiwa kwa namna iliyokusudiwa. Kombo anatupa mfano toka katika shairi liitwalo ‘*UKIMWI Tishio*’ ambapo anasema shairi hili linatupatia sitiari ambayo inajenga dhamira nyingi. Kwa kuchunguza dondoo lifuatalo tunaweza kuthibitisha ukweli huu:

Limetupata ni pigo, janga hili la UKIMWI  
Limechukua uzito, usiokuwa kifani  
Wakubwa pia wadogo, kina mama ni huzuni  
UKIMWI sasa tishio, la maisha duniani

Mapenzi hatari kwako, utaupata UKIMWI  
Kumbuka mzee kifo, wapenzi wakishazidi  
Kulawiti nacho kifo, utavipata viini  
UKIMWI sasa tishio, la maisha duniani

Ukishafahamu hayo, wajibika maishani  
Uamuzi fanya Leo, Kunyoya au kusuka  
Bado UKIMWI ni moto, ndugu zangu tambueni  
UKIMWI sasa tishio, la maisha duniani.

**(UHURU, Januari 27, 1993, Baraka Manyama)**

<sup>2</sup>Kombo anafafanua kuwa mwandishi wa shairi hili ameanza kwa kueleza njia zinazoeza UKIMWI kama vile tabia ya kulawiti na kuwa na wapenzi wengi wasio waaminifu. Mwandishi pia anaeleza madhara ya UKIMWI kuwa ni kifo katika beti mbili za mwanzo. Kwa kutumia sitiari;

<sup>2</sup> Tumechukua maelezo haya katika tasnifu ya uzamili ya Omari Mtunguja Kombo “Kuchunguza Tamathali za Usemi katika Mashairi ya Magazetini: Uchunguzi Kifani wa Mashairi ya UKIMWI katika Magazeti ya Kiswahili,” aliyoiwasilisha kwa ajili ya kutimiza sharti pekee la kutunukiwa shahada ya umahiri katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

“..*Bado UKIMWI ni moto...* “UKIMWI unafananishwa na moto; moto una sifa ya kuteketeza kila kitu. Hali hii inalinganishwa na UKIMWI ambao unaangamiza maisha ya watu. Ni kupitia sitiari hii, dhamira ya madhara ya UKIMWI inaeleweka wazi hasa pale ambapo tunajengewa picha ya moto kuwa sawa na UKIMWI. Kwa ujumla, sitiri zinapotumika katika shairi lolote zinasaidia kukuza na kuifanya dhamira inayoongelewa na mshairi kueleweka kiundani zaidi.

<sup>3</sup>Nao Venance na wenzake (2015) wameshughulikia matumizi ya sitiari na ishara katika ngano ambapo wanaeleza namna tatu za utokeaji wa sitiari katika ngano za Kiafrika: Kwanza wahusika wanaojitokeza kisitiari, pili sitiari kwa njia ya hadithi nzima, na tatu sitiari kwa kutumia maneno ya kulinganisha kama vile: *mfano wa, mithili ya* na kadhalika. Wao wanatupa mifano kutoka ngano mbalimbali zikiwamo hadithi za “Chui”, “Pongo”, “Sungura” na “Fisi”. Vivyo hivyo, ngano hutumia sitiari katika hadithi nzima ambapo msuko wa matukio hujengwa kisitiari kiasi kwamba ili kuelewa hadithi husika ni sharti hadhira ivunjevunje sitiari mbalimbali zilizomo. Venance na wenzake wanatoa mfano wa hadithi za “Dege” na “Kazi kwa Mfalme” ambapo tunaelezwa kuwa sitiari zinazotumika ni ‘safari’, ‘mabonde’ ‘mito’ ‘misitu’ na ‘nyika’. Safari, kwa mfano, inatumika kuwakilisha mchakato wa makuzi ya mwanadamu yaani kuzaliwa, kukua hadi kufa. Maisha ni safari ambayo hukumbana na changamoto na vikwazo vingi ambavyo mwanadamu anatakiwa kupambana navyo ili kufikia kilele cha matarajio yake. Changamoto na vizingi katika maisha ndivyo huwakilishwa kisitiari na mabonde, mito, milima, nyika na misitu minene katika ngano.

Aidha, Nzuki (2003) naye amejaribu kugusia namna sitiari inavyotumiwa na wasanii katika kazi zao, akitumia mfano wa shairi la “Bara Jinge” la Kithaka Wamberia:

Bunge  
Halitakuwa ukumbi  
Wa genge la nzinge  
“Usalama wa taifa”  
Hautakuwa ngozi  
Yakulinda mamba wa ikulu... (uk. 10)

---

<sup>3</sup> Tumechukua maelezo haya katika “Matumizi ya Sitiari na Ishara katika Ngano”, kazi ya wanafunzi wa shahada ya umahiri (M.A. Kiswahili) wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Wanafunzi hao ni Venance Furaha, Margreth Waivyala na Zuhura Katoto. Imetolewa katika mtandao tarehe 22/08/2017 kupitia <http://www.venancefuraha.blogspot.com>

<sup>4</sup>Nzuki anaeleza kuwa mshairi anatumia sitiari kuwarejelea viongozi waovu na waharibufu. Anasema pale mambo yatakapokuwa mazuri kiutawala na hasa baada ya kubadili mfumo wa uongozi, bunge halitakuwa genge (kikundi) la nzige (waovu), na chombo muhimu katika ulinzi wa taifa (usalama wa taifa) hakitakuwa ngozi (kinga) ya kulinda mamba (kiongozi muovu na katili). Kwa kifupi mshairi katika ubeti huu ametumia sitiari ambayo amejenga kwa kutumia taswira; tunaona neno ‘genge’ linawakilisha kikundi, neno ‘nzige’ linawakilisha viongozi waovu, neno ‘ngozi’ linawakilisha kinga au silaha ama zuio, na neno ‘mamba’ limetumika kuwakilisha kiongozi mwovu.

Wataalamu wengi wameshughulikia sitiari katika kazi za kifasihi kama tulivyojaribu kurejelea hapo juu. Imebainika kuwa wasanii hupenda kutumia sitiari kwa namna tofautitofauti, mathalani, sitiari kwa kutumia vilinganishi, sitiari kwa kutumia wahusika, sitiari kwa kutumia mtindo wa hadithi au kazi nzima ya kifasihi. Lengo kuu la makala haya ni kuchunguza matumizi ya sitiari katika mashairi ya msanii Mrisho Mpoto. Kwa maoni yetu, msanii huyu anapenda sana kuandika nyimbo zake katika mtindo wa kisitiari, na hutumia mbinu mbalimbali za sanaa kujenga sitiari katika mashairi yake. Aidha, nyimbo zake zinaelekea kufuata mkondo wa maudhui ya kisiasa, na hasa siasa za Tanzania. Tungo za Mrisho Mpoto zikichunguzwa vizuri ni sitiari ya mwenendo wa siasa na utawala nchini Tanzania na hata kwingineko barani Afrika. Hata hivyo, kabla ya kuanza uchambuzi huo ni vema tukazungumzia walau kwa ufupi juu ya historia ya msanii huyu kwani kuelewa historia ya makuzi yake kutasaidia katika kuelewa tungo zake.

#### **4.0 Historia ya Msanii Mrisho Mpoto**

<sup>5</sup>“Kwanza kabisa nimezaliwa Oktoba 27, mwaka 1978, na kuitwa jina la Mrisho Issa Hussein Mpoto. Mimi ni mwenyeji wa Songea, mkoani Ruvuma nikiwa mtoto wa 36 kati ya watoto 36 wa mzee Issa Hussein Mpoto. Mama yangu Mwanaisha Athumani ni mke wa 12 kati ya wake 12...” Mpoto alinusurika kuuawa mapema kabisa wakati angali mdogo . “Kwa kuwa baada ya mama kunizaa alisema hatazaa tena, kitendo cha kuambiwa anipeleke porini nikafie huko nifukiwe kilimfanya aonekane kama chizi. Mama yangu alikubali kunipeleka porini kwa shingo upande. Usiku akabadili mawazo na kunitorosha kutoka tulipokuwa tukiishi, Mchomoro hadi Namtumbo huku nikiwa naumwa sana...” Mpoto na mama yake waliondoka Namtumbo na kuhamia jijini Dar es Salaam mnamo mwaka 1988 wakati huo yeye akiwa na umri wa miaka kumi tu.

---

<sup>4</sup> Tazama tasnifu ya Uzamili ya Nzuki Permenus Kasilu (2003) “Mwingiliano wa Fani na Maudhui katika Ushairi wa Kithaka Wamberia” aliyoiwasilisha katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

<sup>5</sup> Maelezo haya aliyatoa Mpoto alipokuwa akijibu swali aliloulizwa na mwandishi wa habari wa Global Publishers Limited (GPL) tarehe 23/08/2017.

Mpoti alifanikiwa kuanza masomo katika Shule ya Msingi Ilala Boma, iliyopo jijini Dar es Salaam na katika kipindi hiki cha uanafunzi wake, alianza kuonyesha cheche zake za kisani kwa kuwa alikuwa akishiriki shughuli mbalimbali za kisanaa kama vile maigizo, ngonjera, kuimba na kughani mashairi. Walimu wake walipendezwa na kipaji alichokuwa nacho hata ilipotokea fursa ya usaili wa vipaji kwa watoto, jina lake lilipendekezwa. Mpoti mwenyewe anaeleza kuwa kuna kipindi wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) waliendesha usaili wa kutafuta vipaji vya kuigiza, yeye hakuweza kuhudhuria kutokana na sababu za kiuchumi, anasema: “Nilishindwa kwenda shuleni siku hiyo kutokana na ugumu wa maisha uliokuwa unaikabili familia yangu, hali ambayo ilinifanya nikae nyumbani kumsaidia mama kazi ya kutafuta kuni.” Hata hivyo, kwa kuwa walimu wake walikwisha tambua kipaji cha Mpoti, walipendekeza jina lake na huo ukawa mwanzo wa safari yake ya sanaa. Tangu hapo akawa analelewa kisanaa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Alijifunza sanaa za jadi zikiwamo sanaa za maonyesho ya jukwaani, kughani na kuimba. Juhudi zake katika kuhudhuria mazoezini zilileta mafanikio kwani baadaye alichaguliwa na kituo cha runinga cha ITV kuendesha kipindi cha watoto, na ndipo uzoefu wake ukazidi kuimarika japo hakuwa analipwa chochote. Baadaye Mpoti alipomaliza shule ya msingi na kushindwa kuendelea na masomo ya sekondari aliamua kuendeleza kipaji chake cha sanaa akiwa katika kikundi cha sanaa cha *Parapanda*. Baadaye Mpoti alijiondoa Parapanda kisha akaanzisha kipindi cha mchezo wa kuigiza katika runinga kilichojulikana kwa jina maarufu la *‘Bongo Dar es salaam’* ambacho mhusika wake mkuu alikuwa Kulwa Kikumba maarufu kama *‘Dude’*. Mpoti hakuishia hapo, baadaye alifanikiwa kuanzisha kampuni ya *‘Mpoti Arts Production’* wakiwa na mfanyabiasha mmoja Bw. Tesha, kampuni ambayo iliendelea kufanya kazi za sanaa ya maonyesho kwa mafanikio. Hata hivyo, kutokana na kutokuelewana kati ya wabia wa kampuni hii yaani Mpoti mwenyewe na Bw. Tesha (muwekezaji), kampuni ilivunjika na badala yake Mpoti akaanzisha kampuni nyigine; *‘Mpoti Gallery Theatre’*. Kampuni hii ipo hadi sasa na inajihusisha na sanaa za kiutamaduni, yaani muziki wa asili, maigizo, ngojera, na muziki wa kizazi kipya uliochanganywa na ladha ya asili.

Kwa ujumla, mbali na kipaji cha kuigiza, Mpoti ni msanii mwenye kipaji cha kipekee anayefanya muziki ambao una vionjo vya Kitanzania; ni muziki fulani wenye hadhi ya Kiafrika kifani na hata kimaudhui. Hadi sasa Mpoti amefanya kazi nyingi ambazo zote zimepata kuungwa mkono kwa kiasi kikubwa na hadhira pamoja na ukweli kuwa mtindo wa uandishi wa mashairi autumiao kwa kiasi fulani ni mgumu kueleweka. Tungo zake huwa na maudhui mazito ya kijamii ambayo huwa yamebebwa ndani ya lugha ya picha, ishara, kejeli, chuku, mafumbo na vitendawili. Huyu ni msanii anayejaribu kuipa sanaa

ya uimbaji upya fulani wenye vionjo vya kifasihi simulizi. Nyimbo maarufu za Mpoto ni pamoja na “Nikipata Nauli”, “Asanteni kwa Kuja”, “Adela”, “Chocheeni Kuni”, “Samahani Wanangu”, ”Waite”, “Njoo Uchukue”, “Sinzoje”, na “Kitendawili.”

## **5.0 Tungo za Mpoto: Uchambuzi wa Sitiari ya Mwenendo wa Siasa na Utawala nchini**

Mrisho Mpoto kama tulivyoeleza hapo mwanzo ni msanii anayejipambanua kuwa mwanamuziki wa kipekee kutokana na mtindo wake wa uandishi wa mashairi yake, uimbaji (kughani mashairi), mahadhi na midundo yenye mahadhi ya Kiafrika. Mtindo wa uandishi wa mashairi ya Mpoto ni wa kisasa kama ilivyo kawaida ya wanamuziki wengi nchini, lakini Mpoto hujitofautisha na wengine kwa utajiri wa lugha ya picha, methali, misemo na tamathali za semi katika mashairi yake. Namna yake ya kuimba ni ya kughani mashairi. Aidha, Mpoto anatunga tungo zake kisitiari ambapo anadurusu siasa na utawala nchini. Kazi zitakazoshughulikiwa katika makala haya ni “Njoo Uchukue”, “Sinzoje” na “Kitendawili”. Sababu za kuteua kazi hizi zimekwisha kuelezwa hapo juu.

### **5.1 “Njoo Uchukue”**

Wimbo huu uliimbwa na Mpoto akimshirikisha Felly. Ulirekodiwa na kutolewa mwaka 2015, kipindi ambacho harakati za kampeni za uchaguzi zikiwa zimekaribia na kupamba moto. Hiki ndicho kipindi ambacho wanasiasa hujiandaa kuingia kwenye mapambano ya kuwania nyadhifa mbalimbali za uongozi. Katika mfumo wa kidemokrasia uongozi hupatikana kwa kura; raia huchagua viongozi miongoni mwa wagombea waliojitokeza kuwania nafasi husika; kwa hiyo mshindi ni yule apataye kura nyingi. Mpoto anaanza kwa kuwataarifu wanasiasa kwamba kama kura yake (yangu) itawasaidia kupata ushindi basi waende kuichukua. Katika korasi iliyoimbwa na Felly tunaona maneno haya:

*Eh!*

*Eh!*

*Ohoo Yangu!*

*Kama itakupa ushindi*

*Moyo wako unajua*

*Kama itakusaidia (yangu)*

*Moyo wako unajua*

*Usiku rafiki wa giza*

*(Basi njoo uchukue*

*Basi njoo uchukue*



*Basi njoo uchukue...uichukue)*

Kura ya msanii anayoiita ‘yangu’ inawakilisha kura nyingi za wananchi wa hali ya chini, kura ambazo wagombea wanazihitaji sana ili kufanikisha ushindi wao. Hii ni kwa sababu ya wingi wa kura zenyewe, wananchi wenye kipato cha chini ni wengi nchini. Sauti zao zinapazwa kisitiari na Mpoto, ambaye anaamua kuwaeleza wanasiasa ukweli kuwa kama wanazihitaji kura basi waende kuzichukua. Inaelekea kuwa msanii anaamini kuwa kama wanasiasa wataenda kuzichukua kura nyumbani kwa wananchi basi watapata fursa ya kuona hali ilivyo ngumu huko mtaani na kwamba pengine watakaposhinda watawakumbuka waliowapa ushindi. Katika ubeti wa kwanza Mpoto anaeleza:

*Ama kweli...*

*Kama hujui unakokwenda huwezi kupotea*

*Na watu wakikimbia wanakozika*

*Hudondokea kwenye maiti nyama*

*Siku zote naamini huwezi kulala kwenye mto*

*Hata kama umekauka*

*Na ukitaka kujua mwendo wa mjinga*

*Mpe kilemba uone...*

Hapa tunaona msanii anafunua ukweli kuwa kama mtu hajui aendako basi njia yoyote huweza kumfikisha popote. Inawezekana msanii anatueleza kuwa nchi na viongozi wake hawakujua waendako, matokeo yake tumefika popote kwa njia zozote. Tumekimbia wanakozika na kujikuta kwenye maiti nyama. Msanii ametumia neno ‘maiti nyama’ kisitiari kuwakilisha matatizo yaletayo huzuni kuu, yeye anaona nchi inajikuta kwenye matatizo makubwa baada ya kutoka kwenye matatizo ya awali (wanakozika). Pia, neno “mto” limetumika kisitiari. Mto ni taswira ya hali ya hatari, mlolongo wa shida, matatizo chungu nzima. Msanii anajaribu kutueleza kuwa kamwe mtu hawezi kupumzika wala kukubali kutulia kwenye mkondo wa shida kama vile umaskini na ukosefu wa huduma za jamii. Kiongozi yeyote anayekubali shida hizi ziwapate wapiga kura wake, basi hafai hata kama katika kipindi cha uchaguzi anajitahidi kuukausha mto (kupunguza matatizo) labda kwa kutoa rushwa na kuwadanganya wananchi kwa kuleta baadhi ya maendeleo kama ilivyo kawaida ya wanasiasa ifikapo wakati wa uchaguzi. Kiongozi wa aina hii hubainika pale tu anapopewa madaraka; huyu ni mjinga tunayeweza kumjua kwa mwendo wake baada ya kuvishwa kilemba. Msanii anaendelea kueleza hivi:

*Hili ni ombi langu, toka kwangu kuja kwako*

*Kama ya kwangu itakusaidia chochote*

*Kwenye ushindi wako, niko tayari kukupa  
Ila uifuate nyumbani, wala sio mbali  
Nakukumbusha ukitaka nzi wasikufuate  
Acha kula vilivyoza.  
Chuki humchoma alie hifadhi kwenye moyo*

Msanii anaendelea kutoa ombi kwa wanasiasa kuzifuata kura kwa wananchi, wawatembelee mitaani na mijini na vijijini ili wajionee hali halisi ya maisha yao. Lakini anawapa angalizo viongozi hawa kuwa kama hawataki tuhuma, kashfa na sifa mbaya (nzi) basi waepuke uovu (vilivyoza) katika uongozi wao maana chuki humchoma aliyehifadhi kwenye moyo tu.

Katika ubeti wa pili, Mpoti anatumia kejeli kueleza jinsi wanasiasa wapendavyo kujionyesha mbele za macho ya umma kuwa wanawajali wananchi. Hili tunalishuhudia kila siku kwani viongozi wengi nchini hupenda kufanya kazi mbele ya kamera za waandishi wa habari ili waonekane. Msanii anasema: “...*najua mara nyingi utapenda kuja mchana ili uonekane!*”

Msanii anawaelekeza njia ya kwenda huko anakokuita nyumbani kwake ili wanasiasa waweze kuzifuata kura zitakazowapa ushindi; njia yenyewe inaelezwa kichuku ili kukoleza na kusisitiza ukweli wa mazingira mabovu waishio raia wengi nchini. Msanii anaeleza:

*...Pita uwanja wa taka hadi mfereji mchafu  
Kisha Kibanda cha mbavu za mbwa katiza  
Uisikie la mtu njiani, endelea kuja tu  
Ni kioo tu peke yake,  
Ndo huonesha doa la kweli la mtu kwenye paji la uso  
Katisha choo cha gunia pembeni pembeni maskani  
kempu  
Tariban kempu  
Ukisikia harufu bana pua haraka  
Hapo choo kinapakuliwa  
Nakutia moyo tu, njoo karibia  
Unakaribia kufika*

Tunaona mbali na kuelezwa uhalisi wa maisha ya wananchi, ufukara na uvundo wa maisha duni. Msanii anatumia neno ‘kioo’ kujenga taswira ya wananchi wanaoongozwa kwamba wao ndio waonao na kuonesha kwa usahihi dosari (doa) za viongozi wao.

Ubeti unaofuata unaendelea kueleza njia ya kwenda kuichukua kura ilivyo mbovu na ndivyo watoaji wa kura hiyo waishivyo. Hali hii inaweza kubadilishwa na viongozi wenye utashi pekee. Mpoti anawakaribisha wanasiasa kwenda kujionea mambo yalivyo. Kura za wananchi hazipatikani

kwenye ofisi yenye viti vya kuzunguka na viyoyozi bali hupatikana kule waishiko wananchi, kule kwenye chipisi vumbi, chapati za gengeri, urojo wa ubuyu, pweza na vijiti vyake; kule ambako watu huchangamana na vinyesi na kondomu, dampo huwa jirani na maji ya mtungi; kule wanakotumia vyoo vya pipa; kule ambako watu hawatulii majumbani mwao si kwa sababu wapo kwenye kazi za maana bali wapo mtaani wanaungaunga kutafuta senti ili mkono uende kinywani, maana ajira adimu. Mpoto nasema:

*...kila hatua utakayopiga kumbuka  
Maji ya dafu hayanywewi kwenye glasi  
Na siku hizi kinachopandwa kwenye changarawe  
Kinakua haraka kuliko kwenye udongo*

Mwishoni mwa ubeti huu wa tatu ambao ndio wa mwisho msanii anatumia tashititi pale anapoamua kumhoji mwanasiasa swali ambalo jibu lake kwa vyovyote vile analijua kuwa ni 'ndiyo'. Tashititi hii imetumika ili kujenga hali fulani ya dhahaka ambayo lengo lake ni kufikisha ujumbe kwa mhusika. Wanasiasa hupenda kuchaguliwa lakini husahau hali duni za watu wao; sasa Mpoto baada ya kuwapasha ukweli ulivyo anawapa tashititi ili ujumbe uwakolee barabara. Msanii anauliza: “...Hapo sasa umefika, vipi? Bado unaitaka na ya kwangu ikuongezee ushindi?”

Kwa kuwa jibu ni “ndiyo”, msanii anawapa masharti wawaniaji wa uongozi, masharti yenyewe ni mawili pekee lakini muhimu. Anasema hivi:

*Kama ndiyo, kuna masharti mawili tu  
Pitia kwa yule mama ukamuombe samahani  
Na umpe pole, kwa sababu kwa kauli zako  
Alipoteza kichanga chake  
Na kwenye hela mkiweka picha zenu  
Wekeni na za kwetu  
Wakati mnatumia mtutumie na sisi  
Mwisho lakini si kwa umuhimu  
Kwenye kiapo chako cha kweli  
Ongeza na majina yetu*

Tunaona msanii anatoa masharti; mosi, anamtaka mwanasiasa ambaye hapa anawakilisha wanasiasa na viongozi wote kuwaomba msamaha wananchi kwa kwenda kinyume na ahadi walizozitoa enzi za kuomba kura. Wanapaswa kuwaomba msamaha wananchi kwani kwa kauli zao kama viongozi walisababisha shida kwa wananchi. Ni kweli kumekuwa na kauli mbovu

zitolewazo na viongozi ambazo zingine ni amri zisababishazo madhara makubwa kwa wananchi wa kawaida. Watu wananyanyaswa, wanakandamizwa na kunyimwa haki zao. Kinamama hupoteza vichanga vyao kwa kukosa huduma bora za afya, wakati mwingine kwa sababu ya migomo ya madaktari isababishwayo na kauli mbovu za viongozi.

Pili, msanii anatoa sharti jingine kuwa wakati wa kutumia pesa, wakati wa kufurahia mema ya nchi, wananchi wa kawaida nao wahusishwe “...*na kwenye hela mkiweka picha zenu wekeni na za kwetu.*” Katika kupanga matumizi ya rasilimali za nchi wananchi nao wawekewe bakshishi yao ili ufikapo wakati wa kutumia basi nao watumie, pengine kwa kuimarishiwa huduma za jamii kama vile umeme, maji, elimu, afya na miundombinu. Aidha, mfumo bora wa kiuchumi uundwe kwa kuweka sera nzuri ili kuleta maendeleo kwa watu wote.

Mwisho, lakini siyo kwa umuhimu kama asemavyo msanii, anawataka viongozi wawakumbuke wananchi punde tu wapatapo madaraka ili katika utawala wao wawajali waliowapa madaraka hayo. Anawaambia katika viapo vya uaminifu wakumbuke kuwa nyuma yao kuna orodha ndefu ya watu waliofanikisha kuapa kwao. Hivyo kuapa huko ni kwa watu wote waliowapa madaraka; madaraka na mamlaka ni ya umma, wao ni wawakilishi tu.

“*Njoo Uchukue*” ni sitiari ya siasa na utawala nchini kwani msanii amefaulu kusawiri hali ya mambo ilivyo katika siasa zetu na utawala wetu nchini Tanzania hasa majira ya uchaguzi. Wimbo mzima umejengwa kisitiari tangu mwanzo hadi mwisho. Kuuelewa wimbo huu ni lazima uchambue sitiari zilizomo ndani yake.

## **5.2 “Sizonje”**

“Sizonje” ni wimbo mwingine wa Mrisho Mpoti ambao amemshirikisha msanii Banana Zoro. Wimbo huu ulitoka na kuanza kupigwa kwenye vituo vya redio na runinga mapema mwaka 2016. Ukisikiliza wimbo huu, jambo la kwanza kubaini ni ule mwendelezo wa sitiari ya siasa na utawala nchini, kwani mashairi ya wimbo huu yanaelekea kurejelea kiongozi ambaye alifanikiwa kuifuata kura baada ya kuombwa aifuate nyumbani kwenye wimbo wa “*Njoo Uchukue.*” Msanii sasa anamkaribisha Sizonje (kiongozi) aingie madarakani aone hali ya mambo ilivyo tete. Msanii anaanza kwa kumuelekeza Sizonje kwamba nyumba waishimo kuna vituko na maajabu ya kustaajibisha. Banana Zoro ameimba kipande hicho cha mwanzo kabisa ambacho ndicho korasi ya wimbo huu. Msanii anasema:

*Sizonje hii ndio nyumba yetu  
Milango ipo wanapita madirishani  
Ingia uyaone, maajabu ya nyumba yetu*

Katika kiitikio hiki tunaona msanii amemjenga mhusika wake Sizonje kisitiari kuwakilisha kiongozi mkuu wa taifa na labda ndiye rais. Pia, Sizonje anaweza kuwa kiongozi yeyote mwenye madaraka baada ya kuchaguliwa na wananchi au kuteuliwa na mamlaka mabalimbali. Tunaweza kusema Sizonje wa Mpoto ni rais, waziri mkuu, mkuu wa mkoa, mkuu wa wilaya, mbunge au diwani na hata mwenyekiti wa kijiji au kitongoji. Msanii anaanza kumdokeza kuwa katika nyumba anayoiita ‘nyumba yetu’ kuna maajabu; maajabu hayo ni pamoja na watu kutofuata utaratibu na kutotii sheria za nchi. ‘Nyumba yetu’ inasimama badala ya nchi yetu au jamii yetu au sehemu yoyote yenye utawala pengine kitongoji, kijiji, kata, wilaya, mkoa na kadhalika. Milango inaweza kuwa ni zile taratibu na sheria za nchi, kitendo cha watu kupita madirishani kinawakilisha kutenda mambo bila kuzingatia taratibu na sheria. Kwa hiyo, madirisha ni njia za uchochoro, njia zisizoruhusiwa kisheria kufanya mambo; inaweza kuwa upendeleo, rushwa na ubadhirifu wa mali za umma. Hii ndiyo hali halisi ya mambo aliyoikuta kiongozi nchini. Banana Zoro anaendelea kuimba hivi:

*Tulikaa barazani, tukasikia kelele  
Kelele toka ndani, mtu anaruka dirishani  
Sizonje, karibu nyumbani kwetu, uone maajabu ya nyumba yetu*

Msanii anampasha Sizonje hali ilivyo, watu hukaa barazani (mkutanoni) kujadiliana namna ya kuendesha mambo lakini maamuzi ya vikao hayazingatiwi badala yake viongozi hujifanyia watakavyo tena kwa kuvunja sheria, wanapita zao madirishani. Mpoto anasema:

*Karibu sana Sizonje, hii ndo nyumba yetu,  
Tulipoficha mundu za kupondea wezi.  
Kwani, makaburi yaliyofukuliwa ni lazima yazikwe upya?*

Msanii anamweleza mkuu wa nchi kwa kutumia taswira ya mundu ikiwakilisha pengine silaha za kujihami au ushahidi wa uovu wa viongozi, ushahidi ambao unatosha kuwaweka matatani viongozi waliolihujumu taifa (wezi). Msanii anaamini maovu yaliyokwisha kubainika hayahitaji kufumbiwa macho yaani ni lazima waovu husika washughulikiwe kwa mujibu wa sheria. Labda Mpoto kupitia swali lake “...*Makaburi yaliyofukuliwa ni lazima yazikwe upya?*” anajaribu kumueleza mkuu wa nchi juu ya viongozi ambao walihujumu taifa na kulisababishia hasara katika kashfa mbalimbali kama za Richmond, Escrow, ‘Chenji za Rada’ na kadhalika, kuwa ni sharti wafikishwe kwenye vyombo vya

sheria badala ya kusitiri maovu yao maana makaburi yao yamekwisha kufukuliwa. Mpotu anaendelea:

*Nyumba hii Sizonje ina vyumba vinne  
Vitatu havifunguki,  
Kimoja hakina mlango,  
Japokuwa kina watu ndani  
Na hawaongei Kiswahili.  
Wenyeji wanalala nje na washazoea.*

Hapa tunaona mwandishi anajenga sitiari nyingine kwa kutumia taswira ya vyumba vinne kuwakilisha awamu nne za utawala uliopita, yaani utawala wa Marais Nyerere, Mwinyi, Mkapa na chumba cha nne ni utawala wa Rais Kikwete ambao pengine ndio utawala unaowakilishwa kisitiari na chumba kimoja ambacho hakina mlango licha ya kuwa na watu ndani ambao hawaongei Kiswahili na wanalala sebuleni tena kwa mazoea. Inawezekana msanii anadokeza kuwa katika utawala wa serikali ya awamu ya nne kulikuwa na tabia ya kutosimamia sheria, wageni kutoka nje waliruhusiwa kuja kuchuma mali na kuwaacha wenyeji wakitaabika na ufukara waliouzoea. Kutofunguka kwa vyumba vitatu huenda ni ile hali ya kutochunguzwa, kuhojiwa na kushutumiwa kwa awamu tatu za utawala uliopita. Msanii anaonekana kuwa na dukuduku juu ya vyumba hivi vitatu: Vichafu? Hatujui. Visafi? Hatuna uhakika pia, maana vyumba vimefungwa na havifunguki. Msanii anaendelea kusema yafuatayo:

*Sizonje kule tulipotoka panaitwa jikoni  
Huna haja ya kwenda kule,  
Kumejaa mafundi wa kupika.  
Sasa hivi wanakupikia wewe ili ule ulale,  
Ukiamka muongee,  
Nini hasa ujio na dhima ya safari yako  
Wanashangaa mbona ghafla?*

Msanii anaendelea kujenga sitiari yake ya siasa na utawala kwa kutumia lugha ya picha, taswira na tashititi. Tunaona neno 'jikoni' inawezekana likawa linarejelea ofisi za chama, chama tawala ambacho ndicho kilichomzaa kiongozi huyu Mkuu wa Nchi. Huko wapo wakongwe wa siasa nchini ambao huratibu na kushauri namna ya kuendesha nchi. Mabingwa na vigogo wa siasa hawa kwa mujibu wa msanii wanaonekana kustaajabishwa na kupatikana kwake, tofauti na ilivyotarajiwa. Jambo hili linaweza kuwa linahusu ukweli ulivyokuwa enzi za harakati za kuwania ukuu wa nchi. Wengi hawakumtarajia mshindi kuwa huyu aliyekuja kupitishwa na chama na kuchaguliwa na wananchi. Aidha,

jikoni kunaweza kuwa ni ofisi yoyote ya serikali ambako wataalamu mbalimbali hufanya kazi. Wataalamu hawa ndio wanaonekana kumwandalia mkuu mpya wa nchi chakula (ripoti) ili asome kisha apumzike kabla hawajazungumza naye ili awape mwongozo mpya wa mwenendo wa utawala wake wa serikali ya awamu ya tano. Watu hawa wanahoji mkuu mpya anapenda kazi zifanyike kwa utaratibu upi? Je, ni kwa kufanya kazi bora na nadhifu ama kazi za ubabaishaji kama ilivyozoeleka? Msanii anasema:

*Samahani sana mgeni,  
Wapishi wameniomba kwamba,  
Nikuulize tena kwa kukuomba kwamba,  
Eti unapenda vya mafuta au vya nazi?*

*Wanataka kukuonyesha madoido  
Katika mapishi yao Sizonje...*

Mpoti anamtahadharisha Sizonje wake asiingie kwenye chumba fulani katika nyumba anayo mkaribisha, katika chumba hiki kuna sauti ijirudiayo mara nyingi na tunaambiwa mlangoni pa chumba hicho kulikuwa na picha mbili, moja ni picha na ya pili ni mchoro wa picha ya kwanza. Hii inaelekea ni sitiari ya masuala ya muungano, muungano ambao umekuwa ukilalamikiwa kuwa na dosari kadhaa; labda sauti anazodai msanii kuwa huwa zinajirudia ni malalamiko ya Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar. Mwandishi anajaribu kufananisha picha mbili na serikali mbili zilizopo. Picha ya kwanza huenda ni Serikali ya Muungano na picha ya pili ambayo ni mchoro wa picha ya kwanza basi itakuwa ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Msanii anasema:

*...Na hapa mlangoni kulikuwa na picha mbili kubwa!  
Moja picha, nyingine mchoro wa picha ya kwanza  
Nachokumbuka iliwahi kuandikwa “USIYEMTAKA KAJA”*

Katika mishororo hii mitatu tunaona namna msanii anavyotumia ufundi wake wa lugha kusitiri maana anayokusudia kuiwasilisha ambapo ili kuelewa ni lazima jitihada za kuvunja sitiari zifanyike kama tulivyojaribu hapo juu. Maneno ‘USIYEMTAKA KAJA’ yanadokeza kuwa ujio wa mkuu huyu mpya wa nchi ambaye kwa mujibu wa Mpoti ni ‘asiyependwa’ lakini ndio hivyo kaja. Kutokupendwa kwake kunakomaanishwa hapa kunatokana na kasumba iliyokuwa imejengeka ya kuendesha mambo kinyemela, kwa kujua, kutokufuatwa kwa sheria, na ubadhirifu wa mali ya umma. Anapotokea

kiongozi mwenye kusudi la kuleta nidhamu na uadilifu, wasiompanda lazima wawepo, hasa wale wanaonufaika wa mfumo usio na adilifu.

Mpoto anaendelea kumpasha habari Sizonje; anajaribu kutumia ufundi mkubwa wa lugha hasa misemo na methali kuimarisha ujumbe wake. Msanii anausitiri ujumbe wake katika lugha iliyojaa mbinu mbalimbali za kifani. Pamoja na kuwa “*wimbo mbaya haufai kubembelezea mtoto*” yaani habari zisizo nzuri (wimbo mbaya) hazifai kutumika katika chereko za kufurahia mafanikio fulani au ukaribisho wa kiongozi mpya, Mpoto anaamua kupasua jipu kwa kueleza uovu na matatizo yote yanayolisibu taifa katika siku za mwanzo tu za uongozi wa Sizonje (mkuu wa nchi), siku za fungate ya ushindi. Msanii anasema mtoto (kiongozi mpya) hawezi kuumizwa na mambo au kazi iliyoandaliwa na jamii yake na labda tuseme chama chake kilichomkuza na kumfanya awe kiongozi. Hata hivyo, anatahadharisha kuwa “*harufu ya uzazi haiishi mpaka mtoto akue.*” Yaani madhara ya mfumo uliomlea na kumkuza kama kiongozi hayawezi kukosa. Hayafutiki mpaka pale kiongozi atakapoamua kujisimamia na kujenga misingi imara ya utawala wake nje ya minyororo na kaida za mfumo ulioasisiwa na chama chake Sizonje, mfumo wenye udhalimu mkubwa ambapo serikali imegubikwa na rushwa, hali inayofanya mahakama na magereza yasiwe chochote kwani wahalifu na wahujumu uchumi wa taifa wapo lakini mahakamani hawapelekwi na wala hawafungwi gerezani. Huu ndio mwenendo wa siasa na utawala wa taifa letu la Tanzania, mapapa na manyangumi wa uhalifu dhidi ya taifa hutamba mitaani, daga pekee ndio huswekwa magerezani. Msanii ametumia maneno ‘ua’, ‘shimo la taka’, ‘choo’ na ‘taka’ kisitiari kujenga taswira ya serikali (ua), mahakama au chombo chochote cha maamuzi (shimo la taka), magereza (choo), na wahalifu (taka). Msanii anasema hivi:

*Sawa, Sizonje, huu hapa ni ua, lile pale ni shimo la taka  
Na kile pale ni choo  
Kinachotutisha na kutuogopesha zaidi,  
Wanaoishi humu ndani hawajawahi kutupa taka,  
Wala kwenda chooni*

Vijana wasomi na wasiosoma hulandalanda mitaani wakisaka ajira pasi mafanikio (wanazunguka na ‘bahasha za kaki’), hulalamika lakini malalamiko yao hayasikilizwi. Wazee, kina mama na watoto nao hulalama bila kusikilizwa shida zao. Wanyonge hunyonywa, mathalani, wakulima hunyanyaswa na wanunuzi wa maza, wafanyakazi hulipwa mishahara duni, wafanyabiashara wadogowadogo wakiwamo wamachinga na maman’tilie huvunjiwa vibanda vyao na kufukuzwa na migambo wasipate msaada. Kelele zao zote si chochote si lolote kwa watawala, wao hujali matumbo yao na ya familia zao. Msanii katika kuthibitisha haya anasema:



*...Kama ukiwa makini, kwa nje utasikia sauti za makundi ya watu,  
Wengi ni vijana, wana bahasha za kaki mikononi.  
KAMA HAMTUPI TAKA SHIMO HILI MLICHIMBA LA NINI?*

*Lakini pia kwenye sauti zao,  
Sizonje kuna watoto, wazee na kina mama.  
Ukiunganisha sauti zao ndio unapata hizo kelele*

Sambamba na hayo msanii anatumia kuwa katika taifa hili kuna mambo mengi hufanyika kwa uficho ambayo hasa ni yale yaendayo kinyume na sheria za nchi na ndiyo huwafanya viongozi watambe na kulingia nafasi zao ambazo kamwe hawapendi kuziacha. Kibaya zaidi wafanyao hivi ni tembo (vigogo/viongozi wakubwa) wa nchi hii. Labda kujilimbikizia mali, ardhi, majumba ya kifahari, vitaru vya madini, ukwepaji kodi,— hayo ni baadhi tu ya yanayojiri huko uchochoroni kama asemavyo Mpoto. Msanii anasema haya anapomweleza Sizonje wake:

*...Sasa, njoo nikuonyeshe huku uchochoroni.  
Uone maajabu mengine ya nyumba hii  
Sizonje, ukiona tembo anaringa ujue mvua zinakaribia!*

Tumeona kuwa katika wimbo huu wa ‘Sizonje’ Mpoto anazungumzia masuala kedekede yahusyo mwenendo mzima wa siasa na utawala wa nchi. Msanii amejaribu kubainisha pasi woga matatizo na changamoto nyingi zinazolikumba taifa ambazo hazina budi kushughulikiwa na uongozi mpya wa awamu ya tano chini ya mkuu wa nchi ambaye Mpoto anampachika jina la Sizonje. Mambo kama uongozi dhaifu, uhujumu uchumi au ufiada kama ujulikanavyo leo, utendaji mbovu, rushwa, ukosefu wa ajira, unyanyasaji wa watu wa chini, sera mbovu za kilimo na biashara, upendeleo wa kindugu, utandawazi, na ukoloni mambo yamesawiriwa vyema katika “Sizonje”. Hivyo, tunaweza kusema ‘Sizonje’ inakidhi kuwa sitiari ya mwenendo wa siasa na utawala nchini.

### **5.3 “Kitendawili”**

Huu ni wimbo wa hivi karibuni ambao nao unaelekea kwenye mkondo uleule wa sitiari ya siasa na utawala nchini. Katika wimbo huu, Mpoto amemshirikisha Kassim Mganga. Kupitia wimbo huu msanii anaendeleza falsafa yake ya uongozi unaojali masilahi ya watu wote na kudumisha amali asili za jamii,

falsafa ambayo amekuwa akihubiri karibu katika nyimbo zake zote. Kitendawili ni wimbo uliotoka katikati ya mwaka 2017, kipindi ambacho serikali ya awamu ya tano au tuite serikali inayoongozwa na Sizonje inanza bajeti yake rasmi ya mwaka wa pili ukiondoa ile ya 2015/2016 ambayo kimsingi ni bajeti ya serikali ya awamu ya nne au serikali ya Mjomba kama asemavyo Mpoto. Katika kipindi hiki mambo bado ni fumbo lenye mtego unaohitaji kuteguliwa. Watu wapo katika sintofahamu ya nini ni nini na kipi ni kipi. Hadi sasa hapajawa na mafanikio makubwa ya mabadiliko ya kiuchumi na hali ya maisha ya watu wa kawaida kama ilivyotarajiwa. Watu walikuwa na mategemeo makubwa baada tu ya uongozi wa Sizonje kuingia madarakani wakiamini kila kitu kingeenda sawa mapema tu katika uongozi huu. Matatizo yote aliyobainisha Mpoto katika wimbo wa ‘Sizonje’ yalitarajiwa kwamba yangetatuliwa haraka iwezekanavyo. Jambo linalotia hofu ni kuwa muda unazidi kuyoyoma matatizo yangalipo na mengine mapya yanazuka, ijapokuwa jitihada fulanifulani zinaonekana. Hiki ni kitendawili ambacho mtegeji labda ni Sizonje na wateguaji ni wananchi. Kitendawili ni neno lililotumika kisitari kuwakilisha matendo, hatua, sera na mwenendo wa siasa na utawala wa serikali ya awamu ya tano. Mwenendo mzima wa serikali ya awamu ya tano ni kitendawili kinachohitaji jibu, na jibu lake halijulikani kama ni maendeleo ya watu na taifa kwa ujumla au mwendelezo wa umaskini uliokithiri kwa watu na kuporomoka kwa uchumi wa taifa. Bado jibu lenyewe linabaki kuwa kitendawili. Msanii anasema haya katika korasi inayoimbwa kwa kiasi kikubwa na Kassimu Mganga:

*‘Maji ya moto’  
 Kitendawili tega nikutege  
 Kitendawili tega (tega)  
 Tega nikutege (mwiba)  
 Kuku anaetaga achinjwe  
 Akichinjwa msiba.  
 Sizooonje eh (Sizonje)  
 Sizonje aah eh  
 Sizonje, sizonje eh  
 Kitendawili  
 Sizonje aah eh  
 Sizonje, sizonje eh*

Hapa tunaona msanii anaanza kwa kuitia ari hadhira yake ili iwe tayari kutegua kitendawili cha Sizonje. Maneno ya mwanzo ni ya kawaida yatumikayo kama kianzio cha utegaji wa vitendawili tangu kale, maneno haya hutumika ili kuamsha na kuiweka tayari hadhira kupokea kitendawili na kukitegua. Kitendawili cha msanii hapa ni “kuku anayetaga achinjwe, akichinjwa msiba.”

Hiki ni kitendawili kinachohitaji jibu na ili kukijibu kitendawili hiki ni lazima tutegeue mtego wa swali la kitendawili chake ‘kuku anayetaga achinjwe?’ Ni wazi kuwa kwa mfugaji wa kuku kuchinjwa kuku anayetaga ni hasara kubwa, ni msiba kwa sababu hiyo humaanisha kuwa kuku waliotarajiwa kupatikana baada ya mayai kutotolewa na vifaranga kulelewa vema huwa wamechinjwa pia. Hii ni hasara kuu kwa mfugaji wa kuku. Labda tujiulize mfugaji wa kuku anayezungumziwa hapa ni nani? Je, kuku anayetaga ni nani pia? Kadhalika, je, huo msiba ni wa namna ipi? Maswali haya yanaweza kutusaidia kidogo kuelewa wimbo huu. Inaonekana msanii kama kawaida yake ameficha maana katika kuta za vipengele vya kifani ili kudumisha sitiari yake ya siasa na utawala. Yaelekea kuku ametumika kisitiari kuwakilisha serikali na hatua za mwanzo zinazochukuliwa katika kupambana na changamoto lukuki zinazoliandama taifa. Mathalani, uundaji wa sera madhubuti, utungaji na urekebishaji wa sheria mbalimbali, ufukuzaji wa watendaji na viongozi wabovu, uhakiki wa watumishi, ushughulikiwaji wa mafisadi, uimarishaji wa miundo mbinu, na pengine utoaji wa elimu bure. Huyu ndiye kuku anayetaga na hayo ndiyo mayai yake ambayo yanatazamiwa kutotolewa vifaranga watakaolelewa na kuwa kuku wakubwa tayari kwa kitoweo. Hatua hizi za awali ambazo serikali inachukua ni mayai ambayo yakitunzwa vema kwa joto linalopaswa yatatoa vifaranga na wakilelewa watakuwa kuku. Kwa hiyo, msanii anaona kuwa hatua hizi za Sizonje zikiungwa mkono zinaweza kuleta matunda kwa taifa. Mfugaji wa kuku ni wananchi wote walioipa madaraka serikali iwatumikie. Wananchi wakiamua kutounga mkono juhudi za serikali ni sawa na kumchinja kuku anayetaga,

jambo linaloweza kusababisha kushindwa kufanikiwa kwa azma na nia njema ya kuinua uchumi wa nchi na kuboresha maisha ya kila Mtanzania. Huu ndio msiba wenyewe. Msanii anasema:

*Kumbukumbu yako ikoje katika kukumbuka  
Nilikwita Sizonje ili uingie ndani  
Kwa sababu kila anaye ingia lazima atoke nje  
Sizonje, sizo za nje.  
Hapa ndipo walipobishana,  
Majoho yasiyoonekana,  
Walisoma hapa walimaliza hapa,  
Kila kitu kiliishia hapa.  
Walipokuja kwetu wakatuambia,  
Wale waliosoma na kumaliza,  
Walimaliza kila kitu wakafa,  
Kama hujui bahari ilipo tumia mto kwenda.*

Tunaona kwamba msanii anamkumbusha mkuu wa nchi (Sizonje) juu ya ujumbe wake aliokwisha mweleza awali enzi za ugeni wake katika utawala. Sasa anafafanua kisa cha yeye kumwita ‘Sizonje’ yaani sizo za nje kuwa mamlaka yake ni ya muda mfupi, utafika muda itampasa aondoke; kila anayeingia lazima atoke anasema Mpoto. Aidha, inaonekana msanii anatumia neno ‘majoho’ kurejelea hali ya kuhitimu au kumalizika kwa awamu zilizopita. Anatuambia: “*Waliosoma hapa walimaliza hapa... kila kitu kiliishia hapa.*” Inawezekana msanii anataka kutuambia viongozi waliokwisha maliza awamu zao za utawala walihudumu na kustaafu kazi pale ikulu na baada ya kuondoka madarakani kila kitu kikakoma pale maana hawana tena nafasi na mamlaka kama awali. Zamu zao ziliisha wakatoweka. Kilichobaki sasa ni wengine wanaoshika hatamu kuongoza kwenda kunako maendeleo kwa watu wote, na kama haijulikani namna ya kufika huko, basi njia mbadala ya kufuata nyayo za viongozi bora itumike. Msanii anaendelea kusema:

*Kiukweli watu wanalilia,  
Wapo wanaolia kwa machozi  
Na wapo wanaolia kimya kimya,  
Wapo wanaolia na wanaoendelea kulia  
Japo vilio vinatofautiana.  
Wapo wanaolia kwa kuhisi wamedanganywa,  
Wapo wanaolia kupoteza ndugu zao,  
Lakini wapo wanaolia kuona kuna msiba kwao  
Lakini marehemu ndio mwandaaji.  
Wali mweupe kwa sheikh  
Usiweke nyama za mifupa  
Watoto kaeni wanne wanne  
Waandaji tutakula uani tena mwisho...*

Msanii anamweleza ukweli Sizonje wake kuwa kwa kushika kwake hatamu, watu wanalilia vilio vyenye sababu tofauti. Baadhi ni kwa sababu ya kupoteza ndugu zao pengine kutokana na kufukuzwaji wa wafanyakazi na viongozi waovu na wazembe kunakofanyika. Wengine wananung’unika kwa kuhisi wamedanganywa hasa baada ya kuona ahadi zilizoahidiwa hazitimii na muda unayoyoma. Hii inaweza kuwa ni kutokana na ukweli kuwa zipo ahadi hazijatekelezwa kwa wakati kama ilivyotazamiwa. Mathalani, kutatua tatizo la ukosefu wa ajira za kutosha, kufuta tatizo la masilahi duni ya wafanyakazi, kumaliza tatizo la unyanyasaji wa wafanyabiashara wadogowadogo, na labda kuinua na kujenga uchumi wa viwanda. Wapo pia wanaolia kuona msiba kwao na mwandaaji ndio marehemu, yaani wale ambao rais ametokana na chama chao wanaumia kuona masahibu yakiwapata ndugu na jamaa zao wa chama

chao wakishughulikiwa kwa makosa yao katika mamlaka pasi kujali wanatoka chama kipi. Ile tabia ya kubebana na kufichiana uozo kwa mgongo wa ukada inapofifia, waliozoea lazima waumie. Neno ‘marehemu’ limetumika kisitiari kuwakilisha wapotevu yaani waliofukuzwa kazi baada ya kwenda kinyume na sheria; msiba ni ile huzuni na uchungu unaokuja baada ya kuondolewa madarakani kwa marehemu. Mpoti anadokeza pia suala la elimu kuwa ni muhimu na vyema iendeleo kutolewa bure maana watoto wanahitaji kupata elimu bora bila kujali hali zao za kimaisha. Mwisho msanii anahoji jambo linalofaa kati ya kusitisha hatua za kiutendaji zikiwamo zile za kufukuza wasiofaa, au kuendelea kuchunguza na pale inapobainika udhaifu basi walio sababisha (maiti zinazotembea) washughulikiwe hata kama vilio vinazidi kuongezeka. Msanii anasema haya kuthibitisha:

*Shida zilivyohamia shuleni,  
Nikaona nikuwahi kidogo Sizonje,  
Mtoto mdogo anapoulizwa nani atalipa ada  
Baba, yuko wapi? Kafa.*

*Mwalimu wa fasihi,  
Anapotoa mfano wa maiti zinazotembea  
Wale watoto wanalia tena.  
Kwa hiyo Sizo huku nje watu wote wanalia tofauti  
Lakini msiba ni mmoja, unaonaje?  
Tuzike kwanza, au tuhesabu idadi ya maiti zinazotembea?*

Msanii anaona kuwa ukali na ukatili unaweza kusababishwa na tabia za kichokozi. Chui ametumika kisitiari kuwakilisha tabia ya ukorofi, ukatili na ukali ambao unadhaniwa kuwa mkuu wa nchi anao. Tunaambiwa yawezekana wanaouchagiza ni watu kwa tabia zao za uzembe na ujanjaujanja katika kutenda kazi, jambo ambalo halimpendezi mkuu. Aidha, tunaambiwa anayekunyoshea kidole kuwa makini naye muda si mrefu atakunasa kofi; yaani anayetia chokochoko na vurumai ni wa kuangaliwa kwa makini kwani muda wowote anaweza kusababisha maumivu au anguko. Kupitia msemu huu Mpoti anadokeza umuhimu wa kujizatiti dhidi ya hila zinazoweza kuleta mtikisiko ama kuporomoka kabisa kwa utawala. Nani anamnyoshea kidole? Labda ni wale wanaopinga baadhi ya hatua zichukuliwazo na serikali. Msanii anasema:

*Naomba ikumbukwe kwamba  
Aliyemfundisha chui kula watu  
Ni binadamu*

*Na anaye kunyoshea kidole  
Kuwa makini naye, sio muda mrefu atakunasa kofi...*

Mwisho, msanii anahitimisha kwa kutoa mtazamo wake juu ya mwenendo wa siasa na utawala wa serikali ya awamu ya tano nchini, ambapo anaelekea kuamini kuwa pamoja na ukweli kuwa hali ya maisha imezidi kuwa ngumu mtaani kutokana na kupungua kwa mzunguko wa fedha, hali inayofanya biashara kuwa ngumu na karibu kila shughuli ya uzalishaji kupungua, wananchi wanapaswa kuwa wavumilivu wasubiri hatua zinazochukuliwa zilete matokeo: "...kuku atotoe vifaranga na mayai viza yabainike." Msanii anaona haja ya kusubiri hata kama hali ngumu ya maisha iliyopo imewachosha wananchi kwani ili mambo mazuri yatokee ni sharti kungojea hatua zinazochukuliwa na misingi imara inayowekwa isubiriwe hadi itakapoleta tija: "...inawezekana kweli tumechoka maharage lakini kama tunataka nyama tusebiri kwanza banda lijae." Mpoto anatwambia hivi:

*Kuku ana hatua tatu katika ukuaji wake,  
Hatua ya kwanza atage,  
Tujue utagaji na wingi wa mayai yake  
Tunamsubiri atotoe,  
Tuhesabu vifaranga na mayai viza.  
Ndugu zangu,  
Inawezekana kweli tumechoka maharage  
Lakini kama tunataka nyama,  
Tusebiri kwanza banda lijae.*

Msanii amefikia hitimisho hili labda kutokana na dalili zinazoonisha kuwa baadhi ya hatua na maamuzi yanayofanyika yanaelekea kujenga misingi imara ya uchumi, mfano suala la kuhimiza uchumi wa viwanda, kuimarisha utendaji kazi na nidhamu kazini, kujenga uadilifu, kushughulikia sheria na mikataba ya madini. Kwa vyovyote vile, Mpoto amejitahidi kudurusu nyendo zote za siasa na utawala wa nchi huku akikosoa, kuonya na kupongeza mambo mbalimbali.

## **6.0 Hitimisho**

Mrisho Mpoto ni msanii ambaye amejipambanua kuwa muumini na mfuatiliaji mzuri wa siasa na utawala wa nchi kwani ameweza kuzunguka kona zote za siasa na utawala si tu katika nyimbo tatu zilizochambuliwa katika makala haya bali pia katika nyimbo zake nyingine nyingi. Ukichunguza vizuri nyimbo za Mpoto tangu "Salamu Zangu Mjomba" hadi huu wa "Kitendawili", utabaini kuwa nyimbo zake zote zipo katika mkondo uleule wa kuzungumzia siasa na

utawala wa nchi. Mbinu yake ni ileile ya kutumia sitiari ya jumla ambapo mashairi yake yote huyajenga kisitiari kusawiri siasa za nchi. Kwa mfano, katika wimbo wa “Salamu Zangu Mjomba” aliomshirikisha Sanga, Mpoto anatuma barua kwa Mjomba ambaye ndiye Mkuu wa Nchi akimkumbusha shida za wananchi. Inaelekea Mjomba hakisikia na wala hakujibu barua ile. Kwa sababu hiyo, Mpoto akaamua kuomba nauli katika wimbo uliofuata wa “Nikipata Nauli,” akimweleza tena mjomba kuwa akipata nauli ataenda kuonana naye ana kwa ana wazungumze *amweleze* magumu wayapatayo ndugu zake aliowasahau. Pengine nauli ilipatikana Mpoto akasafiri akisindikizwa na ndugu jamaa na marafiki, akaeleza tena masaibu fulanifulani na mafanikio ya safari yake hiyo katika “Asanteni kwa Kuja”. Bado hali iliendelea kuwa mbaya Mpoto akaamua sasa kumtuma binamu yake katika wimbo wa “Adela”, mtoto wa mjomba, aende kumweleza kinagaubaga baba yake ambaye ndiye mjomba wake Mpoto juu ya utete wa mambo ulivyo. Hata hivyo, inaonekana bado mambo yalizidi kwenda mrama, yakazuka na mengine likiwamo la mgogoro wa Muungano. Hapo Mpoto akamshauri mengi ili kusuluhisha jambo hilo katika wimbo wa “Waite”. Mgogoro huo ni kama uliisha lakini bado hali ya kimaisha iliendelea kuwa tete, mambo yakawa shaghalabaghala; wenye nacho walineemeka na wengine wakazidi kutaabika. Mpoto akaamua kuwaasa wananchi kuhamasishana ili kumshinikiza Mjomba asawazishe mambo. Akawaambia wachochee kuni ili chakula kiive. Haya tunayapata katika wimbo wa “Chochea Kuni”. Chakula kiliiva au hakikuiva haijulikani, lakini akawafunda wananchi wasitoe kura kirahisi hadi pale anayeitaka imuongeze ushindi. Akamwambia mhitaji wa kura aende kuichukua katika wimbo wake wa “Njoo Uchukue.” Kura ilifuatwa, mshindi akapatikana. Mpoto akamkaribisha nyumbani na kumsimulia mambo ya ajabu katika nyumba na kisha akampachika jina jipya la Sizonje kwa kuwa huyu ni mwingine hakuwa Mjomba wake tena (katika wimbo wa “Sizonje”). Kutokana na ujio wa Sizonje kuleta sintofahamu katika minong’ono ya watu, Mpoto anaamua kutega “Kitendawili” kila mmoja ategue. Jibu linabaki kuwa kitendawili, maana Sizonje ni Kitendawili vilevile.

## **Marejeleo**

Global Publishers (2010). “*Simulizi ya Mrisho Mpoto: Mahojiano kati ya Mwandishi wa Habari na Mrisho Mpoto*” katika <https://globalpublishers.co.tz>

Kombo, M.O. (2014). “Kuchunguza Tamathali za Semi Katika Mashairi ya Magazetini: Uchunguzi Kifani wa Maishairi ya UKIMWI katika

- magazeti ya Kiswahili.” Tasnifu ya Uzamili (Umahiri). Haijachapishwa. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Mpoto, M.H.I. (2015). *Wimbo wa “Njoo Uchukue.”* Haujachapishwa.
- Mpoto, M.H.I. (2016). *Wimbo wa “Sizonje.”* Haujachapishwa.
- Mpoto, M.H.I. (2017). *Wimbo wa “Kitendawili.”* Haujachapishwa.
- Msokile, M. (1992). *Misingi ya Hadithi Fupi.* Dar es Salaam: Dar es Salam University Press.
- Msokile, M. (1993). *Msingi wa Uhakiki wa Kifasihi.* Dar es Salaam: East Africa Education Publishers.
- Mulokozi, M.M na Kahigi, K.K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani yetu;* Dar es Salaam: TPH
- Mwakio, L.W. (2016). “Matumizi ya Tashibiha, Sitiari na Taashira Katika Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.” Tasnifu ya uzamili. Haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Nzuki, P.K. (2003). “Mwingiliano wa Fani na Maudhui Katika Ushairi wa Kithaka wa Mberia.” Tasnifu ya Uzamili. Haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Samwel, M na wenzake (2013). *Ushairi wa Kiswahili, Nadharia, Maendeleo, Mwongozo kwa Walimu wa Kiswahili na DIWANI YA MEA.* Dar es Salaam: MEVELI Publishers.
- Venance, F na wenzake (2015). “*Matumizi ya Sitiari na Ishara*” katika [Venancefuraha.blogspot.com](http://Venancefuraha.blogspot.com), imetazamwa kwa mara ya mwisho tarehe 22/08/2017
- Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na na Nadharia.* Nairobi: Focus Publishers.